## UTANGULIZI

Tume ya Pamoja ya Fedha ni Taasisi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyoundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 134 na kuanzishwa kwa Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya mwaka 1996, Sura 140.

Muundo wa Tume ya Pamoja ya Fedha una Ngazi kuu tatu (3) za kiuongozi na kiutawala ambazo ni Makamishna, Sekretarieti na Menejimenti.

Majukumu ya Tume ya Pamoja ya Fedha yameainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara 133 na 134. Kwa mujibu wa Ibara hizo, majukumu hayo ni yafuatayo:-

- Kuchambua Mapato na Matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano na kutoa Mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgawo wa kila mojawapo wa Serikali hizo;
- Kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za kifedha wa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili;
- Kutekeleza majukumu mengine ambayo Rais ataipatia Tume au kama Rais atakavyoagiza, na kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Katika kutekeleza majukumu hayo, Tume imekuwa ikizingatia utawala bora mahala pa kazi. Aidha, Katika kufikia malengo ya Maendeleo ya Taifa Serikali imekuwa ikisisitiza utawala bora ili kukuza na kuimarisha amani na utulivu, ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii na kupunguza umasikini. Utawala Bora umesisitizwa na kuimarishwa katika sekta muhimu kwa



kutekeleza maboresho mbalimbali katika sekta ya umma ukiwamo Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya kwanza (I), ya pili (II) na ya tatu (III). Mikakati hiyo imekuwa ikiainisha aina za rushwa na athari zake katika jamii kama ifuatavyo:-

## MAANA YA RUSHWA

Rushwa ni fedha au kitu cha thamani kinachotolewa au kupewa mtu mwenye madaraka ya jambo fulani ili mtoaji apatiwe upendeleo. Pia rushwa ni matumizi mabaya ya madaraka kwa manufaa binafsi.

## AINA ZA RUSHWA

Kwa mujibu wa Taarifa ya utafiti kuhusu vyanzo vya rushwa iliyotolewa na Tume ya Rais ya Kero za Rushwa (PCIAC) ya mwaka 1996 ilibainisha njia kuu mbili za namna rushwa inavyoweza kujidhihirisha nchini ambazo ni:-

1. Rushwa katika Mifumo ya Utawala (Rushwa ndogo)

Hii inahusisha watumishi wa Serikali na mawakala wao kudai rushwa kwa wananchi kwa huduma zinazotolewa bure.

2. Rushwa Kabambe (Kubwa)

Inahusisha viongozi wa ngazi za juu Serikalini wenye mamlaka ya kutoa maamuzi, kupitia Sera na Mikataba.

### ATHARI ZA RUSHWA

Baadhi ya athari za rushwa mahala pa kazi ni:-

- Kuzorota kwa kazi
- Kushuka morali ya kazi
- Kukosekana kwa haki



Baadhi ya athari za rushwa kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ni:-

- Huathiri misingi ya utawala bora, utawala wa kisheria na demokrasia.
- Husababisha mgawo usio sawa wa rasilimali za Taifa.
- Husababisha kukosekana kwa haki.
- Wananchi kukosa imani na Serikali yao.
- Huleta matabaka ya walionacho na wasionacho.
- Serikali kushindwa kutekeleza miradi ya maendeleo.
- Husababisha vifo.

## MALENGO MAHSUSI YA MKAKATI WA TAIFA DHIDI YA RUSHWA AWAMU YA TATU (2017-2022)

Mkakati wa Taifa dhidi ya rushwa Awamu ya Tatu una malengo mahsusi yafuatayo:-

- Kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji wa utoaji wa huduma katika Sekta ya Umma na Binafsi.
- Kutekeleza kwa ufanisi Mikakati ya mapambano dhidi ya rushwa.
- Kuzijengea uwezo Taasisi simamizi za mapambano dhidi ya rushwa na
- Kuwa na uongozi madhubuti wa kisiasa katika mapambano dhidi ya rushwa.

Mkakati huu umelenga kupunguza na kudhibiti rushwa katika sekta/ maeneo muhimu ya kimkakati ambayo ni pamoja na manunuzi ya umma, ukusanyaji wa mapato, utoaji wa haki, maliasili na utalii, madini, nishati, mafuta na gesi, afya, elimu na ardhi.

## TUME YA PAMOJA YA FEDHA INAVYOSHIRIKI UTEKELEZAJI WA MKAKATI DHIDI YA RUSHWA AWAMU YA TATU

Tume inawajibika kutoa huduma kwa wadau mbalimbali bila upendeleo. Katika kufanikisha azma hiyo, imeweka mazingira wezeshi ya kuzuia na kupambana na rushwa na matendo yaliyo kinyume na maadili ya utumishi wa umma kama ifuatavyo:-

- Imeunda Kamati ya Uongozi ya Usimamizi wa masuala ya uadilifu mahala pa kazi ambayo ndiyo mratibu wa kazi zinazotekelezwa na Kamati ya Kudhibiti Uadilifu,
- Imeunda Kamati ya Kudhibiti Uadilifu mahala pa kazi,
- Imeweka utaratibu wa kutoa zawadi kwa mtumishi yeyote atakae wezesha kupatikana taarifa zitakazo thibitisha uwepo wa rushwa na kutotaja jina la mtoa taarifa,
- Imeweka sanduku la maoni linalo tumika kutoa taarifa yoyote iliyo kinyume na maadili ya utumishi wa umma.

## NAFASI YA WATUMISHI KATIKA KUTEKELEZA MKAKATI WA AWAMU YA TATU DHIDI YA RUSHWA

- Kutoa taarifa mapema katika Kamati ya Kudhibiti Uadilifu yanapojitokeza mazingira yaliyo kinyume na maadili ya utumishi wa umma ikiwamo rushwa.
- Kutoa taarifa katika mamlaka zilizopewa jukumu la kupambana na kuzuia rushwa (TAKUKURU) pindi anapobaini rushwa au viashiria vya rushwa sehemu



yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Kufanya kazi kwa uadilifu kwa kuzingatia Sheria, Taratibu, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya utumishi wa umma.
- Kuelimisha jamii kuhusu rushwa, madhara na mapambano dhidi yake.
- Kutumia sanduku la maoni kutoa taarifa na malalamiko kuhusu rushwa.

## HITIMISHO

Tume itaendelea kuwawezesha watumishi wake kupata elimu dhidi ya rushwa ili washiriki ipasavyo katika mapambano hayo. Aidha, wakati wote Tume itawahamasisha watumishi wake kutekeleza majukumu yao katika mazingira ya uwazi kwa kuzingatia Sheria, Taratibu, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya utumishi wa umma.

Tume ya Pamoja ya Fedha itaendelea kushirikiana hususan na Taasisi ya Kupambana na Kudhibiti Rushwa nchini (TAKUKURU) na Serikali yote kwa ujumla katika kuhakikisha malengo ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (2017 - 2022) yanafikiwa.

Tume ya Pamoja ya Fedha
Jengo la Sukari - Mtaa wa Ohio/ Barabara ya Sokoine
S. L. P. 9281
**DAR ES SALAAM**
Email: katibu@jfc.go.tz
Tovuti: www.jfc.go.tz

Tume ya Pamoja ya Fedha
Jengo la ZSTC – Mtaa wa Gulioni
S. L. P. 1796
**ZANZIBAR.**
Email: katibu@jfc.go.tz
Tovuti: www.jfc.go.tz



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME YA PAMOJA YA FEDHA

## UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA DHIDI YA RUSHWA AWAMU YA TATU (2017-2022)

**Nafasi ya Tume katika kutekeleza Mkakati**

**Nafasi ya watumishi kufanikisha Mkakati**

**APRILI, 2021**